

CLASS 6 END TERM 3 MARCH 2022

KISWAHILI

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya uliyopewa.

Malezi ___ 1 ___ ya mtoto hutegemea mambo kadhaa. Ni sharti mtoto ___ 2 ___ maadili tangu akiwa ___ 3 ___. Licha ya maadili, ni vyema aidha mtoto aelekezwe katika kumtambua ___ 4 ___ wake kupitia kuonyeshwa njia ya ibada ___ 5 ___. Tena, mtoto ___ 6 ___, hana budi kupewa mahitaji ya kimsingi kama vile ___ 7 ___. Elimu bora aidha huwa haki ya mtoto. Haya yakizingatiwa, watoto wetu watainukia kuwa kizazi kikamilifu na chenye mtazamo bora ___ 8 ___.

1. A. nzuri B. mema C. jema D. mbaya
2. A. alazimishwe B. aonyeshewe C. aandamishwe D. afuatane
3. A. nyumbani B. tumboni C. shuleni D. mchanga
4. A. mwalimu B. muumba C. mzazi D. mtoto
5. A. makanisani au misikitini B. makanisani na misikitini
C. hekaluni na darasani D. misikitini na nyumbani
6. A. anapolelewa B. anapolewa C. anapolewalewa D. anapoelewa
7. A. chakula, nguo na tarakilishi B. elimu, ulinzi na matibabu
C. lishe, mavazi na maskani D. nyumba, nguo na michezo
8. A. kwa maisha B. kwenye maisha C. katika maishani D. maishani

Sisi ___ 9 ___ tulimfahamu Mariamu kuwa msichana mwenye bidii masomoni, hata ___ 10 ___ na kukosa kuja shuleni kwa siku nne, tulienda hospitalini ili kumjulika hali. Hospitalini, alikuwa amelazwa katika ___ 11 ___ ya wanawake. Daktari alikuja na ___ 12 ___ na kupenyeza dawa kupitia begani pake. Baada ya kumtia moyo, ___ 13 ___ huyo alisema kuwa siku iliyofuata ___ 14 ___ kuondoka maana alikuwa amepata ___ 15 ___.

9. A. sote B. zote C. wote D. zozote
10. A. alipogonjeka B. alipoungua C. alipokuwa D. alipoungua
11. A. machela B. wodi C. mochari D. kitanda
12. A. machela yenye mashuka B. sanda yenye maua
C. sirinji yenye sindano D. kitabu chenye maandishi
13. A. nesi B. mganga C. mama D. mwanamume
14. A. ataruhusiwa B. asingeruhusiwa C. ameruhusiwa D. angeruhusiwa
15. A. hasara B. dawa C. nafuu D. mauti

- Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali kulingana na maagizo.**
16. **Karibu** imetumikaje katika sentensi ifuatayo?
Fuliza na dada yake wako karibu kufika.
A. Umbali B. Idadi
C. Wakati D. Nusura
17. Chagua sentensi yenye kivumishi kiashiria radidi.
A. Ndege hizo ndizo za kijeshi.
B. Bilauri hizi hizi ndizo za mama.
C. Miche ii hii ndiyo iliyopandwa jana.
D. Mgonjwa yule alitibiwa akapona.
18. Kitenzi **sema** katika hali ya kutendeka huwa
A. semea B. semesha
C. semwa D. semeka
19. Chagua ulinganifu unaoonyesha kitenzi kilichoundwa kutokana na nomino.
A. Matangazo - tangaza.
B. Pika - mapishi.
C. Ujasiri - jasiri.
D. Mpole - wapole.
20. Chagua orodha yenye viungo vya mapishi **pekee**.
A. Sufuria, birika, jiko.
B. Dania, pilipili, kitunguu.
C. Pilau, pure, ugali.
D. Nyanya, chumvi, mayai
21. Nomino **miadi** iko katika ngeli ya
A. U - I B. I - ZI
C. I - I D. U - ZI
22. Kanusha sentensi hii:
Kutembea kwingi, kujua mengi
A. Kutotembea kwingi, kujua mengi.
B. Kutembea kwingi, kutojua mengi.
C. Kutotembea kwingi, kutojua mengi.
D. Kutembea kwingi si kujua mengi.
23. Chagua sentensi yenye **ka** ya mfuatano wa vitendo.
A. Tuliomba tukaanza safari.
B. Walienda uwanjani wakacheza.
C. "Njooni!" mwalimu akasema.
D. Nendeni nje mkacheze.
24. Jibu la **alamsiki** ni
A. buriani dawa.
B. binuru.
C. inshallah.
D. jaala.
25. Chagua zana ya vita iliyo tofauti na nyingine...
A. Kombora B. Bomu
C. Mzinga D. Mkuki
26. Kutokana na nomino **kilimo** tunaweza kuunda nomino
A. lima.
B. limishwa.
C. wakulima.
D. limalima.
27. Badili sentensi ifuatayo katika hali ya wingi **Kufuli hili ndilo langu**.
A. Makufuli haya ndilo yangu.
B. Makufuli haya ndiyo yangu.
C. Kufuli hili ndilo letu.
D. Makufuli haya ndiyo yetu.
28. Tumia kiulizi -pi ipasavyo. **Chumbani mlimofagiliwa ni**
A. kipi?
B. mpi?
C. wapi?
D. kupi?
29. Mtu **mjamzito** ni yule
A. asiye mwepesi kwa uzani.
B. aliye na mtoto tumboni.
C. mwenye lugha ya adabu.
D. asiye na mimba.
30. 9:45 ni saa
A. kumi kasorobo.
B. tatu na robo.
C. tisa na robo.
D. nne kasorobo.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 hadi 40.

Paka na mbwa walikuwa wanyama waliokuwa majirani. Wanyama hao **walipendana kama chanda na pete**. Mara nyingi, watoto wao walicheza pamoja wakati wazazi wao walipoenda shambani kupalilia migomba na kuwinda. Mbwa alipenda sana kuwinda kuchakulo na nguchiro huku paka akiwa stadi wa kuwakamata panya. Jioni baada ya mawindo, wangetayarisha chakula chao pamoja, nje katika mbalamwezi. Wakati huo, watoto wao wangecheza kwa furaha na kuwaongeza wazazi kuni huku wakisubiri chakula kiwe tayari.

Siku moja, wanyama hao walipokea mwaliko kutoka kwa kaka mbweha, mnyama aliyeishi peke yake katika nyika ya Majuto. Maana hawakutaka kuandamana wote ugenini, waliwaaga wana wao saa tatu kamili asubuhi na **kung'oa nanga**. Walipofika, kaka mbweha aliwapokea kwa moyo mkunjufu na mikono miwili. Aliwaelekeza hadi sebuleni mlimokuwa na zulia maridadi, runinga kubwa ya kisasa na makochi yaliyobonyea bonyebonye. Baada ya kaka mbweha kuviingiza viatu vyao humo nyumbani, aliwawashia runinga na kuwapa gazeti la siku hiyo ili wajue habari za nyikani. Paka alimwomba kaka mbweha kitenzambali, kisha akachagua kipindi cha vibonzo kilichoitwa Akiji. Huku paka akiendelea kukifurahia kipindi cha Akili, mbwa aliiteremsha miwani yake na ikaukalia uti wa pua yake na kufurahia ripoti za gazetini.

"Haya ndugu zangu, niwaandalie nini?" Kaka mbweha aliuliza kwa furaha. Mbwa aliomba achemshiwe mifupa ya nyati atafune na kuteremsha kwa supu huku paka akiagiza maziwa baridi ya ngamia na mayai ya kenge.

- | | |
|---|--|
| <p>31. Ni wanyama wangapi waliotajwa katika ufahamu?
A. Watatu.
B. Wanne.
C. Wawili.
D. Watano.</p> <p>32. Walipendana kama chanda na pete ni mfano mmoja wa
A. nahau.
B. tashbihi.
C. istiaru.
D. chuku.</p> <p>33. Shughuli za paka na panya zilizusu
A. matembezi na ulaji.
B. malezi na kilimo.
C. uwindaji na kilimo.
D. kilimo na matembezi.</p> <p>34. Kulingana na aya ya kwanza,
A. paka na mbwa walipenda kuwawinda nguchiro.
B. watoto wao walizoea kupika pamoja.
C. mbwa alikuwa hodari wa kuwashika panya.
D. kuchakulo walikanatwa na mbwa.</p> <p>35. Ni kina nani walikuwa na jukumu la kuongeza kuni?
A. Watoto wa paka na wa mbwa.
B. Wana wa paka.
C. Watoto wa mbwa.
D. Wazazi wa watoto hao.</p> | <p>36. Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kusema kuwa wanyama hao
A. waliishi kwa kuchukiana.
B. hawakuwajali watoto wao.
C. waliishi kwa furaha kuu.
D. walipenda kuwatembelea marafiki.</p> <p>37. Kung'oa nanga ni
A. kumaliza shughuli.
B. kuanza safari.
C. kupanga ziara.
D. kwenda kwa kasi.</p> <p>38. Sebuleni mwa kaka mbweha hamkuwa na
A. gazeti.
B. zulia.
C. runinga.
D. redio.</p> <p>39. Chagua sifa moja ya kaka mbweha.
A. Mchoyo.
B. Mkali.
C. Karimu.
D. Maskini.</p> <p>40. Paka aliagiza chakula gani?
A. Sharubati.
B. Mayai.
C. Mifupa.
D. Supu.</p> |
|---|--|

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 hadi 50.

Siku ya wapendanao inakaribia. Tangu mwaka huu ulipoanza, wengi wamekuwa wakisubiri kwa hamu na ghamu tarehe kumi na nne Februari itimie. Katika siku hii muhimu, ahadi nyingi zilizowekwa hutimizwa huku wapendanao wakitiana moyo kwa njia mbalimbali. Ni siku ambayo zawadi kochokocho hubadilishanwa. Mara nyingi, utawaona watu wa matabaka mbalimbali wakiwa wamevalia mavazi mekundu na kujipamba zaidi kwa kubeba mawaridi mekundu. Wengine hutembea wakiwa wameshikana mikono kama ishara ya mapenzi.

Wakati huu, mtoto anaweza kuwazawidi wazazi wake kwa kuwanunulia mavazi maridadi au kuwaandalia karamu. Wazazi aidha wanaweza kuadhimisha siku hii kwa kuwakilisha wana wao kwa ajili ya nasaha maalumu. Ni kwingi tumewahi kushuhudia wanafunzii wakiwaletea walimu wao zawadi katika siku hii muhimu. Walimu kadhalika wanaweza kuwaletea wanafunzi wao zawadi mbalimbali katika siku hii. Hata wazazi wanaweza kubadilishana zawadi.

Kinyume na fikira za wengi, siku hii hailengi kundi fulani tu la watu. Vikundi mbali mbali vya watu vinaweza kuitumia siku hii kukumbukana na kuifanya uhusiano wao kupata upya fulani. Hata waliojengeana chuki wanaweza kutumia siku hii kusameheana, kukumbatiana na hata kubadilishana zawadi. Je, inawezekana kwa vigogo wa mashirika mbali mbali kuithamini siku hii kwa kuwapa wafanyakazi wa mashirika hayo marupurupu ili waufurahie uhusiano wao na kuongeza bidii kazini?

- | | |
|--|--|
| <p>41. Kulingana na ufahamu, wengi wamekuwa wakisubiri nini tango mwanzoni mwa mwaka?
A. Wapendanao.
B. Tarehe nne Februari.
C. Siku ya wapendanao.
D. Sherehe ya kusameheana.</p> <p>42. Kulingana na msemaji, ni rangi gani hutamalaki wakati wa siku ya wapendanao?
A. Nyeupe B. Nyekundu
C. Samawati D. Nyeusi</p> <p>43. Ni gani hapa si kawaida kutendwa katika siku hii?
A. Kutiana moyo B. Kupeana zawadi
C. Kusameheana D. Kujenga chuki</p> <p>44. Kulingana na taarifa, wafuatao wanaweza kubadilishana zawadi ila
A. vigogo wa mashirika na wafanyakazi.
B. baba na mama.
C. wazazi na watoto.
D. walimu na wanafunzi.</p> <p>45. Fikira za wengi kulingana na taarifa ni kuwa siku ya wapendanao
A. huweza kuboresha uhusiano.
B. ni siku ya kupeana zawadi.
C. hulenga kundi fulani la watu.
D. haiadhimishwi humu nchini.</p> | <p>46. Kwa mujibu wa taarifa, ni kina nani wanaweza kupokea zawadi ya mawaidha? ·
A. Wazazi B. Maadui
C. Wafanyakazi D. Watoto</p> <p>47. Chagua kauli isiyo kweli kulingana na taarifa.
A. Siku ya wapendanao huwahusu wachumba tu.
B. Msamaha huweza kupatikana siku hii.
C. Sherehe inayozungunziwa husherehekewa mwezi wa pili.
D. Maua mekundu huipamba zaidi siku yenyewe.</p> <p>48. Kulingana na taarifa, kukumbatiana kunaweza kuwa ishara ya
A. kujengeana chuki.
B. kusameheana.
C. kuondoa mapenzi.
D. kuongeza hasira.</p> <p>49. Wanaoonekana wakishikana mikono watembeapo huonyesha
A. ulinzi B. ujasiri
C. kinga D. mapenzi</p> <p>50. Taarifa hii inastahili mada gani?
A. Siku ya mawaridi mekundu.
B. Siku ya wapendanao.
C. Sherehe ya msamaha.
D. Sherehe ya wanandoa.</p> |
|--|--|